

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA



**Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,  
Baraza la Madiwani.**

**TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA  
MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA (JULAI –  
SEPTEMBER) MWAKA WA FEDHA 2022/2023 KWENYE KIKAO  
CHA TAREHE 11/11/2022**

## **1.0. UTANGULIZI**

**Mhe. Mwenyekiti,** Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani kwa kutoa Taarifa ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila Robo ya Mwaka. Hivyo, Taarifa hii itagusa Maeneo yafuatayo:-

- i. Taarifa ya Mhe. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzindua Stendi ya Mabasi na Malori Nyamhongolo.
- ii. Taarifa ya Makusanyo kwa robo ya kwanza.

- iii. Taarifa ya mapokezi ya vitabu vya kiada
- iv. Taarifa ya ziara ya mafunzo ya Madiwani na Wataalam kutoka Halmashauri ya Mji Nzega.
- v. Taarifa ya fedha za mapato ya ndani zilizopelekwa kwenye miradi ya Maendeleo
- vi. Taarifa ya ujenzi wa maboma ya shule za Msingi

## **2.0. TAARIFA ZA MATUKIO MBALIMBALI.**

- i. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mnamo Tarehe 13/09/2022 Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe, Dk. Philip Isdor Mpango alifika kuzindua rasmi Stendi ya Mabasi na maegesho ya Malori Nyamhongolo.
- ii. **Mheshimiwa Mweyekiti**, Halmashauri kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 imefanikiwa kukusanya jumla ya TSh.5,016,854,151.61 sawa na asilimia 37.1 ya makisio ya bajeti ya mwaka 2022/2023 ambayo ni mapato ya ndani, kati ya hayo mapato halisi ni Tsh. 4,971,454,979.63 sawa na asilimia 38.1 ya bajeti na mapato fungwa ni Tsh. 45,399,171.98 sawa na asilimia 9.8 ya bajeti.
- iii. **Mheshimiwa Mweyekiti**, Mnamo Tarehe 20/09/2022 Halmashauri imepokea kutoka Taasisi ya Elimu (TET) jumla ya vitabu 24,114 kwa ajili ya shule za Msingi na Sekondari ambapo kati ya hivyo, vitabu 18,328 ni kwa ajili ya shule za sekondari na 5786 ni kwa ajili ya shule za msingi

- iv. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, mnamo tarehe 12/10/2022 wahe, Madiwani na Wataalam kutoka Halmashauri ya Mji Nzega walifika katika Halmashauri yetu katika ziara ya mafunzo ambapo walitembelea Stendi ya Mabasi na Malori Nyamhongolo kwa lengo la kujifunza na kupata uzoefu.
- v. **Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa robo ya kwanza, kiasi cha shilingi 890,277,544.26 zilielekezwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika kata zetu kwa mchanganuo ufuatao:


<b>SEKTA</b>	<b>MIRADI</b>	<b>KIASI TOLEWA (TSH.)</b>
<b>UJENZI</b>	Umaliziaji wa Jengo la Utawala	123,969,499.04
	Mradi wa matofali	65,672,592.00
	Kuwezesha uwekaji wa mradi wa umeme katika soko la muda la Magomeni	3,347,614.33
	Kuwezesha matengenezo ya barabara ya mtaa Bwiru ziwani	7,000,000.00
<b>Jumla ndogo Ujenzi</b>		<b>199,989,705.37</b>
<b>ELIMU MSINGI</b>	Ununuzi wa madawati kwaajili ya shule ya msingi	34,406,328.00
	Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya msingi Kangaye	54,000,000.00
	Ujenzi wa matundu 20 ya vyoo shule ya msingi Lukobe	20,000,000.00
	Ukamilishaji wa darasa shule ya msingi Kiloleli	12,500,000.00

<b>Jumla Ndogo Elimu Msingi</b>		<b>120,906,328.00</b>
<b>ELIMU SEKONDARI</b>	Utengenezaji wa vitanda shule ya sekondari ya wavulana Bwiru	7,500,000.00
	Ukamilishaji wa bweni la shule ya sekondari ya wavulana Bwiru	58,000,000.00
	Ujenzi wa mashimo ya vyoo katika shule ya sekondari Bujingwa	4,821,060.00
<b>Jumla ndogo Elimu Sekondari</b>		<b>70,321,060.00</b>
<b>AFYA</b>	Ujenzi wa Zahanati kata ya Kawekamo	50,000,000.00
	Ujenzi wa wodi ya akina mama katika kituo cha afya Buzuruga	50,000,000.00
<b>Jumla ndogo Afya</b>		<b>100,000,000.00</b>
<b>MAENDELEO YA JAMII</b>	Kuwezesha mfuko wa wanawake, vijana na walemavu	194,762,139.19
<b>ARDHI</b>	Fidia ya ardhi maeneo ya shule za Sekondari Nyasaka, na Lumala	204,298,311.70
<b>JUMLA</b>		<b>890,277,544.26</b>

- vi. **Mheshimiwa Mwenyekiti;** Tumefanikiwa kukamilisha ujenzi wa maboma 45, ofisi 4 na matundu ya vyoo 4 katika baadhi ya shule za Msingi. Hii ni kuwapongeza wananchi na viongozi katika maeneo haya kwa jitihada zilizofanywa kama inavyoonekana kwenye Jedwali;

S/N	JINA LA KATA	IDADI YA MABOMA YA MADARASA	IDADI YA OFISI	IDADI YAMATUNDU YA VYOO
1.	BUGOGWA	10	02	-
2.	KAHAMA	07	-	4
3.	KAWEKAMO	04	-	-
4.	SHIBULA	07	02	-
5.	BUSWELU	03	-	-
6.	NYAMHONGOLO	04	-	-
7.	KISEKE	01	-	-
8.	BUZURUGA	02		
9.	NYAMANORO	04		
10.	BEZI	03		
<b>JUMLA</b>		<b>45</b>	<b>04</b>	<b>4</b>

*Mheshimiwa Mweyekiti, naomba kuwasilisha.*



Eng: Modest J. Apolinary

**MKURUGENZI WA MANISPAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**